# Ugonjwa wa kifua kikuu unakuathiri vipi wewe?



Idara ya Afya ya Massachusetts
Mgawo wa kifua kikuu
2003

# Ugonjwa wa Kifua Kikuu ulimwenguni leo



**Watu millioni ishirini ni wagonja kila mwaka**
**Watu millioni tatu hufa kila mwaka**

# Ugonjwa wa Kifua Kikuu ni nini?



**Ni ugonjwa**

**ambao unasababishwa**

**na kijidudu**

**ambacho kinaingia**

**ndani ya mapafu**

**mtu anapo**

**pumua.**

## Ugonjwa wa Kifua Kikuu una hatua mbili:



**Kuambukizwa kifua kikuu**



**Ugonjwa wa Kifua Kikuu**

# Kuambukizwa Kifua Kikuu



## Vijidudu

- ❑ Vilivyo hai lakini ambavyo havijaanza kushambulia mwili
- ❑ Vilivyozzungukwa na chembechembe ambazo hukinga mwili kutokana na magonjwa

## Mtu

- ❑ Si mgonjwa
- ❑ Hawezi Kuambukiza

# Ugonjwa wa Kifua Kikuu



## Vijidudu

- ❑ Vimeanza kushambulia mwili na kuongezeka
- ❑ Vimeanza Kudhuru mwili

## Myu

- ❑ Anajiskia mgonjwa
- ❑ Anaweza kuambukiza wengine

# Nini hasa husababisha maambukizo ya kifua kikuu Kikua na hata kuwa ugonjwa?



**Ukuta wa chembe chembe zinazokinga mwili Kutokana na magonjwa huporomoka kutokana na kufifia kwa kinga mwilini**

## Nini husababisha kufifia kwa kinga mwili?

- ❑ Ukosefu wa lishe bora
- ❑ Wasiwasi
- ❑ Matumizi ya madawa ya kulevya
- ❑ Kuambukizwa ukimwi *
- ❑ Matumizi ya dawa za matibabu
- ❑ Umri mchanga na uzee
- ❑ Matatizo mengine ya kiafya

# Dalili za ugonjwa kifua kikuu

- ❑ Koohzi
- ❑ Kupungua uzani
- ❑ Uchovu
- ❑ Kutokwa na jasho usiko
- ❑ Homa

# Ugonjwa wa kifua kikuu unaweza kupatikana katika schemu zote zamwili wako



**Vijidudu vinavyosababisha kifua kikuu vinaweza kuenezwa iwapo mtu mwenye vijidudu**




**Unaweza kuambukizwa kifua kikuu iwapo utakaa katika chumba kimoja na mtu kama huyu kwa muda mrefu.**

# Vijidudu vya kifua kikuu haviwezi kuenezwa kwa:

- ❑ Kukutana kwa muda mfupi
- ❑ Kutumia vyombo pamoja
- ❑ Kutamia vitambaa vya kufutia pamoja
- ❑ Kushika chakula

## Kuna ukaguzi ile ujue kama umeambukizwa kifua kikuu

### Njia ya kukagua ngozi ya mtu ya PPD



### Je, ni muhimu kukaguliwa kama una kifua kikuu?

# Ndio, Iwapo...

- ❑ Unashi au kufanya kazi katika mazingira yenye watu wengi
- ❑ Umekaa na mtu ambaye alikuwa anaugua kifua kikuu
- ❑ Iwapo kinga yako ya mwili ni dhoofu
- ❑ Kama ulikuja Amerikani kutoka nchi ambayo ina watu wengi wanaougua kifua kikuu
- ❑ Unatumia madawa ya kulevya
- ❑ Unafanya kazi ya afya ya jamii

# Kumbuka



**Lazima urudi ili ngozi yako ikaguliwe!**

# Iwapo utakuwa na vijidudu baada ya ukaguzi wa PPD; basi inamaanisha:



- ❑ Umeambukizwa kifua kikuu
- ❑ Unahitjii kupaigwa picha ya kifua
- ❑ Unahitaji kutumia dawa za kutibu

**Lakini hamaanishi unaweza kueneza vijidudu vya kifua kikuu**

# Dawa za kifua kikuu

- ❑ **Ndio njia ya pekee**
  **ya kuua vijidudu**
  **vinavyosababisha**
  **kifua kikuu**




- ❑ **Tumia dawa hizo**
  **kwa muda ambao**
  **dahtari amekuagiza**
  **kuzitumia**

- ❑ **Piga ripoti kwa**
  **daktari wako**
  **iwapo kuna shida yoyote**

# Chanjo ya BCG

- ❑ Inatumika ulimwenguni kote kuzuia kifua kikuu kwa watoto
- ❑ Huwa haitumiki kwa wingi Amerikani
- ❑ Haina uhakika wa kuzuia ugonjwa wa TB
- ❑ Huwa inaweza ikaonyesha kama una vijidudu iwapo utafanyiwa ukaguzi wa PPD

# Saidia Kuzuia Kuenea Kwa Ugonjwa Wa Kifua Kikuu

- ❑ Fungua madarisha ili hewa safi iingie
- ❑ Funika kinywa unapokohoa
- ❑ Dumisha mienendo ifaayo ya afya

**Wafunze wengine yale ambayo unayajua**